

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



28 APRILI, 2022



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA KUMI NA NNE – TAREHE 28 APRILI, 2022

I. DUA

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA MADINI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

## **MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko huo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

### **III. MASWALI:**

#### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

##### **108. MHESHIMIWA FRANCIS ISACK MTINGA (IRAMBA MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali inatumia vigezo gani katika mgawanyo wa Watumishi wapya kwenye Halmashauri hususani Walimu.

##### **109. MHESHIMIWA LEAH JEREMIAH KOMANYA (MEATU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ya ujenzi wa Daraja la juu Mto Semu katika Kijiji cha Mwamanongu Meatu.

### **OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

#### **110. MHESHIMIWA DKT. CHARLES STEPHEN KIMEI (VUNJO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuingia kwenye biashara ya Gesi Joto (Carbon Trading).



### **WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

#### **111. MHESHIMIWA REHEMA JUMA MIGILA (ULYANKULU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itawapatia uraia Wananchi 6000 kutoka Burundi waliokamilisha mchakato wa maombi ya uraia Jimbo la Ulyankulu.

**112. MHESHIMIWA MOHAMED JUMAH SOUD (DONGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali inatumia Vigezo gani kuanzisha Vituo vya Polisi katika maeneo ambayo idadi ya watu na vitendo vya kihalifu vinaongezeka.

**WIZARA YA KILIMO:**

**113. MHESHIMIWA MAIMUNA SALUM MTANDA (NEWALA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali imejipangaje katika kuondoa changamoto ya ucheleweshwaji wa viuatilifu kwa Wakulima wa zao la Korosho.

**WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:**

**114. MHESHIMIWA ALLY MOHAMED KASSINGE (KILWA KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara:-

Je, mazungumzo ya Serikali na Wawekezaji kujenga Kiwanda cha Mbolea Kilwa Masoko kwa kutumia Gesi Asilia yamefikia hatua gani.

**115. MHESHIMIWA ENG. STELLA MARTIN MANYANYA (NYASA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Kituo cha SIDO Wilayani Nyasa.

**WIZARA YA MAJI:**

**116. MHESHIMIWA BONIPHACE NYANGINDU BUTONDO (KISHAPU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itapeleka maji ya Ziwa Victoria kwenye Kata 24 zilizopo katika Tarafa tatu Wilayani Kishapu.

**117. MHESHIMIWA BONIPHACE MWITA GETERE (BUNDA):**


Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, mpango wa kupeleka maji ya Ziwa Victoria  
kutoka Bunda Mjini kwenda Vijiji 33 vya Tarafa  
ya Chamriho umefikia hatua gani.

**IV. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha  
Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya  
Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.



**DODOMA**

**28 APRILI, 2022**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc***  
**KATIBU WA BUNGE**